## KANISA KAMA MWILI MMOJA WA KRISTO

Yesu aliagiza wanafunzi wake kwenda kuhubiri injili duniani kote na kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi wake(**Math 28:19-20**; **Mark 16:15-16**). Kuhubiri injili ni kazi ya **uinjilisti** wakati kuwafanya kuwa wanafunzi wake ni kazi ya **ualimu**. Lakini pia kwa mamlaka ya jina la Yesu, wafuasi wa Yesu walipewa mamlaka ya kuponya magonjwa, kufukuza mapepo, n.k (**Mark 16:17-20)**. Lakini tujiulize kuwa ni wote waliompokea Yesu wanatoa mapepo? Au wanaponya wagonjwa? Au ni waalimu? Au ni winjilisti? Kama jibu ni **hapana**, ni kwanini? wakati maandiko yanasema '***kila mliombalo kwa jina langu mtalipokea'***? (**Math 20:22**; **Yoh 14:13-14**).

Yesu aliahidi kuleta msaidizi wa kweli (Roho Mtakatifu) ambaye ndiye atakayekuwa kiongozi na mwalimu katika kuwaongoza wafuasi wa Yesu katika kuitenda kazi aliyowaachia (**Mdo 1:8; Yoh 14:26, 16:13**). Lakini huyo Roho atamgawia kila mtu karama tofauti tofauti katika kuujenga mwili mmoja wa Kristo (**1Kor 12; Rm 12**).

Hivyo huduma mbalimbali na matendo ya miujiza yanayofanyika sehemu mbalimbali na watumishi walioitwa kwa jina la Yesu ni utendaji kazi wa karama tofauti tofauti za Roho Mtakatifu. Ni kweli kuwa wengine wanatumia nguvu za giza lakini wapo wanaofanya kazi ya Kristo (**Mark 9:38-40**). Tulifanye neno liwe nuru yetu ktk kila jambo (**Zab 119:105; Yoh 17:17-19**)

### KARAMA ZA ROHO MTAKATIFU

#### Karama za Roho Mtakatifu ni Nini?

Kabla ya kujua maana ya Karama za Roho Mtakatifu ngoja tujue maana ya neno **Kipawa na Karama. Kipawa** ni uwezo ambao mtu aliozaliwa nao ambao humwezesha kufanya jambo fulani vizuri au kwa ufanisi Zaidi ya wengine (Kamusi ya Kiswahili Sanifu). Ipo mifano mbalimbali ya vipawa kama vile wachezaji wa mpira, kwamba wote wanaweza kuwa wanacheza mpira uwanjani lakini kuna wengine wana uwezo zaidi ya kufundishwa na kocha wao. Wachezaji kama vile Ronaldo Dilima, Lionel Messi, Ronadinho, Diego Maradona n.k uwezo wao uwanjani ulikuwa hautegemei kocha. Pia wapo waimbaji wa nyimbo za dini na za kidunia wenye vipaji tofauti tofauti, wapo pia watu wenye vipaji vya akili n.k

**Karama** ni **Kipawa** ambacho Mungu **kupitia Roho Mtakatifu humzawadia** mtu kwa **neema** kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo. Karama za Roho Mtakatifu kwa mfano karama za nguvu (karama za kuponya, karama za matendo ya miujiza, karama ya uvuvio) humpa mtu uwezo/kibali cha kuomba haja kwa Mungu na kukubaliwa mara moja; kibali cha kupokewa haja iombwayo moja kwa moja, mfano kutoa mapepo, uponyaji n.k.

Katika kamusi ya kiswahili kwa kiingereza, neno '**karama**' limetafsiriwa kama **gracious gifts** likiwa na maana ya **zawadi za neema**. '**Neema**' ni kustahilishwa bila kustahili au bure. Kwa hiyo zawadi za neema ni zawadi ambazo mtu anazipata bila kustahili au kuzigharimia. Maana yake mtu anapata zawadi kwa sababu ***aliyempa ameamua kumpa*** na kwamba anaweza kunyimwa yeye na akapewa mwingine na hawezi ***kudai kwa sababu siyo haki yake***.

Kwa maana hiyo, **karama za Roho Mtakatifu** ni zawadi ambazo Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu anawapa wakristo waliookoka kwa neema kwa ajili ya kulijenga kanisa lake (**1 Petro 4:10**). Karama ni vipawa kwa sababu uwezo huo anaoupata mtu si wa kawaida na si wote wanaweza kuwa nao isipokuwa wale tu waliopewa; ni zawadi kwa sababu mtu yeyote (mkristo/mwamini aliyeokoka) anaweza kupewa kama Roho Mtakatifu apendavyo na si haki ya kudai upendavyo. **Karama** ni uwezo wa kiroho ndani ya mtu wa kutenda kazi ya Bwana. Au ni uwezo wa utendaji kazi wa Roho mtakatifu ndani ya mtu baada ya kuokoka. Ni madhihirisho ya utendaji kazi wa Roho Mtakatifu ndani ya mtu aliyeokoka.

Karama za Roho Mtakatifu hazifanyi kazi kwa ajili ya mtu binafsi bali kwa ajili ya kulijenga kanisa na si kwa mapenzi ya mtu binafsi bali kwa mapenzi ya Roho."Lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye" **(1Kor 12:11).** ***Hivyo maandiko hayadokezi hali tofauti za kiroho kwa watu wenye karama tofauti tofauti na wasiyonavyo ilihali wameokoka*** ila maandiko yanadokeza kuwa tutake karama zilizo za kuu Zaidi **(1Kor 12:31)**, yaani zile ambazo Roho Mtakatifu anapendezwa mwamini Fulani awe nazo**.** Kwa hiyo ieleweke kuwa watu wawili wanaweza kuwa wameokoka lakini wasiwe na karama zinazofanana na hivyo kati yao yule asiye na karama fulani asijione kuwa yeye siyo wa rohoni na wala yule mwenye karama fulani asijione yeye ni wa rohoni zaidi. Lakini pia ili karama mbalimbali ziweze kufanya kazi vizuri ndani ya muumini, ni lazima kiwango chake cha utakatifu kiwe kizuri kwa sababu Roho Mtakatifu hawezi kufanya kazi ndani ya mtu ambaye hana ushirika mzuri wa kiroho.

Roho Mtakatifu ndiye huamua ampe nani zawadi gani bila kujali mpokeaji kuwa anapenda au hapendi karama hiyo. Mkristo akiwa mwaminifu mbele za Mungu, Roho Mtakatifu atampa karama kama apendavyo Roho yeye mwenyewe (**1Kor 12:8**). Kila mmoja kwa kadri alivyoipokea karama, anatakiwa kuitumia kwa kuhudumiana...." (**1 Petro 4:10**). Kwa nini tuwe na karama mbalimbali katika kanisa? Ili kulijenga kanisa" (**1Kor 14: 12**) hivyo tunapaswa kutamani kuwa nazo na kuzifahamu (**1Kor 12:1**) ili kulijenga kanisa. Kwa hiyo ili hizi karama zifanye kazi vizuri ndani yetu ni lazima (1) Tuzifahamu (2) Tuwe na shauku na utayari wa kufanya kazi na Roho Mtakatifu.

**MAMBO MUHIMU KTK KARAMA ZA ROHO MTAKATIFU**

- Ipo tofauti kati ya huduma na karama. Huduma ni wito kwa watu fulani kutumika eneo fulani la kiroho. Karama ni zawadi kwa wote waliookoka. Hivyo karama hufanya kazi ndani ya huduma ya mtu na asiye na wito wa huduma fulani.

- Karama zinaweza kuja na kufanyakazi pale tu Roho Mtakatifu anapoona inafaa na zinaweza ondoka pale uhitaji huo unapokoma, Siyo kitu cha kumiliki **(Mdo 18:27-28)**.

- Fahamu na kubali kwamba karama za Roho zinaweza kufanya kazi hata kwako (**Rm 12:3-6).** Hizi karama ni zawadi kwa kwa wale waliompokea Kristo ili kuujenga mwili wa wake siyo mali ya watu fulani**.**

- Karama za Roho Mtakatifu zinatolewa kwa waliookoka tu **(Mark 16:17-18**) hivyo wapagani wana vipaji vya kuzaliwa siyo karama za Roho Mtakatifu.
- Kila aliyeokoka anaweza kupewa aina fulani ya karama za Roho Mtakatifu ila siyo kila aliyeokoka ana hizo karama kwa sababu ni Roho wa Mungu anayegawa kama apendavyo yeye mwenyewe (**Mdo 11:27-28, ms 22,13:2, 9:32-34, ms 38).** Hivyo kila aliyeokoka anatakiwa kuzitaka hizo karama kufanya kazi ndani yake.
- Ili karama za Roho Mtakatifu ziweze kufanya kazi ya muumini, ni lazima awe na hamu ya kutaka msaada wa Mungu kupata hayo madhihirisho ya Roho Mtakatifu (**1Kor 14:1, 12-13**)
- Kwa kadri ya imani yako karama zitatenda kazi vizuri (imani yako ni muhimu sana): Karama hutenda kazi ndani ya mtu kutegemeana pia na kiwango cha imani alichonacho. Unapokuwa na imani kubwa na thabiti, karama za Roho Mtakatifu zinatenda kazi Zaidi (**Rm 12:6).** Ukifahamu Neno la Kristo kwa wingi utaamini na kutembea katika karama kwa kadri ya imani hiyo (**Rm 10:17**).
- Jifunze jinsi roho anavyowasiliana na wewe: mawasiliano baina ya Roho Mtakatifu na mkristo (aliyeokoka) hayako mbali kwa sababu mbalimbali, kwanza mkristo ni hekalu la Mungu; pili, Roho Mtakatifu anakaa ndani ya mkristo (**1Kor 3:16**). Hivyo ni muhimu kujua jinsi hizi karama zinavyofanya kazi ili kuongeza ushirika wako na Roho Mtakatifu. Madhara ya kutojua utendaji kazi wa hizi karama ni kwamba mtu anaweza kuona kama vile Mungu hamtumii kwa kazi yake na hivyo anaweza kujikataa yeye mwenyewe na kupunguza ushirika wake na Mungu.
- Kuendelea kukua kiroho: Tunapaswa kulikulia neno, imani na maombi kila wakati, hii ikiwa ni pamoja na kutegemea nguvu za Roho Mtakatifu katika kila jambo tunalolifanya na hata tunalopanga kufanya. Kuna kiwango cha nguvu za Roho Mtakatifu ndani ya mtu ambacho hakiwezi kusukuma karama fulani za Roho Mtakatifu kufanya kazi au kuhudumu; tunahitaji kukukua kiroho na kutaka kujazwa tena Roho Mtakatifu kila mara.
- Karama hukoma kufanya kazi mara tu mwenye karama anapoachana na uwezo wa Roho Mtakatifu (**1Tim 4:16)** kwa hiyo ni vyema mwenye karama ajitahidi kuwa mchaji wa neno la Mungu daima (**1Kor 2:12-13).** Lakini pia ni vyema ifahamike kuwa kutofanya kazi kwa karama fulani ndani yako haimanishi kuwa kiwango chako cha kiroho kimeshuka. Kumbuka hizi karama hufanya kazi kadri Roho mwenyewe atakavyo na hivyo inawezekana kabisa ipo karama fulani ambayo Roho Mtakatifu alikutumia kwa siku fulani au kipindi fulani tu.

- Viongozi wa kanisa wanayo nafasi ya kuchochea (**2 Timotheo 1:6**) kuibua karama na kukuza karama kwa njia ya malezi kamili ya neno pamoja na kupewa fursa ya kutumika kwenye huduma (**1Tim 4:14-16, ms 15; Rm 12:6)**

**AINA MBALIMBALI ZA KARAMA**

Zipo aina mbalimbali za karama lakini Roho ni yeye yule, pia zipo huduma tofauti tofauti na Bwana ni yeye yule.

Neno la hekima, Neno la maarifa, Imani, Karama za kuponya, Matendo ya miujiza, Unabii, Kupambanua roho, Aina za lugha, Tafsiri za lugha, Masaidiano, Maongozi, (**1Kor 12:4-5**,**12:28**).

Huduma, Kufundisha, Kuonya, Utoaji (kukirimu), Kusimamia (uongozi), Rehema (Huruma) **(Rm 12:6-8**).
Hakuna orodha kamili inayotaja karama zote za Roho Mtakatifu, kwa sababu Roho wa Mungu anawawezesha watu kwa kadri ya mabadiliko ya hali ya uhitaji, wakati na mahali tofauti (**Mdo 13:2; 1KOR 12:7, 11; Gal 2:9; 1Tim 4:14**).

**KARAMA 9 (1Kor 12)**

Zimewekwa katika makundi 3

1. KARAMA ZA KUNENA

   Kundi la karama hizi hutumia kinywa cha mwanadamu hivyo mwanadamu anaweza kutumia karama hizi kwa makusudi yake: mfano kusema neno ambalo siyo la Roho Mtakatifu.

   - **Unabii**: maana ya unabii (**1Kor 14:1, 31**) hapa ni kama karama hii haijatumika pamoja na karama zingine bali imesimama yenyewe. Ni kuhutubu, yani kusema maneno yanayojenga wengine kwa msaada wa Roho Mtakatifu, kuonya, kuthibitisha maneno yale ambayo Mungu tayari ameshasema nawewe, kufariji n.k. Karama hii haihusiani na kutabiri mambo yajayo. Watumishi wengi hutumika eneo hili ambapo ambapo Mungu huwapa maneno ya kunena na watu moja kwa moja saa ile ile. **Unabii kama huduma**: hutokea pale ambapo karama ya unabii inapotumika pamoja na karama zingine hasa karama za ufunuo kwa muda wote. Hata hivyo nabii hana mamlaka wala uamzi wake yeye mwenyewe kumfanyia mtu unabii mpaka pale Roho mtakatifu anapomwelekeza kufanya hivyo.
   - **Aina za Lugha**: Siyo ile lugha ya kunena ambayo mtu hunena kama ishara ya kumpokea Roho Mtakatifu. Hivyo asiache kunena kwa kisingizio kwamba yeye hana karama ya aina za Lugha. Karama za lugha zinaweza kuwa za lugha za malaika ama wanadamu. Mara nyingi zimewatokea watu ambao wanahudumu

mazingira fulani hivyo katika kuomba kwao wakajikuta wale watu wa lugha tofauti kabisa wakielewa yale maombi ya kunena tena katika Lugha yao wenyewe.

- **Tafsiri za Lugha**: Mara nyingi huambatana na karama za lugha ambapo mtu mmoja hupewa karama za kunena na mwingine kupata tafsiri hapo hapo.

2. KARAMA ZA UFUNUO
   - **Neno la maarifa**: Siyo maarifa ya kusoma au kujua au kutafsiri neno, siyo ule ufahamu wa kawaida wa kujua neno au mapenzi ya Mungu. Karama hii inahusisha kupewa kujua jambo fulani kuhusu wewe (mfano: kujua hila zilizojificha juu ya utumishi wako), mtu mwingine (mfano: kujua shida au uhitaji alio nao mtu fulani bila hata yeye binafsi kukueleza/kuvaa hali ya mtu mwingine katika moyo wako), mahali, tukio lililotokea au linalotokea au litakalotokea ili uweze kufanya maamuzi sahihi (**Mark 2:5-8; Lk 3:15-18, 20:20-23**). Aina hii ya karama huambatana kwa ukaribu sana na karama ya neno la hekima. Angalia utambuzi wa Anania kwa Sauli (**Mdo 9:10-14**). Pia angalia ufunuo wa Petro kuhusu Anania na Safira **(Mdo 5:4-5**), angalia habari ya Gehazi mtumishi wa Elisha alipochukua zawadi kutoka kwa Naamani (**2Waf 5:25-27**). Maono (kupewa mafunuo nje ya utambuzi wa akili zako za kawaida), ndoto, kutokewa na malaika, mawazo (mawazo ya utambuzi wa kiroho) vyote ni mfano wa neno la maarifa (**Yoeli 2:28-30). Ukiwa mwaminifu mbele za Mungu, mwombe akupe uwezo wa kusikia na kutii sauti yake kisha mambo yote haya yatakuwa dhahiri kwako.**
   - **Neno la Hekima:** Siyo hekima ya kupambanua maneno au ujuzi wa dunia na mambo yake **(1Kor 2:6-13)**. Karama hii inafanya kazi kwa karibu sana na karama ya neno la maarifa. Ni hekima ya kupewa ufunuo wa mpango wa Mungu kwa mambo yajayo kuhusu mtu, wewe binafsi, mahali, nchi n.k. Hukupa majibu ya maswali ambayo kibinadamu huna majibu yake na baadaye mtu akikuuliza uliwezaje kufanya jambo fulani hata wewe hakika huwezi kujua nini kilitokea (**Mt 10:19-20, Lk 21:14-15**). Ili kufahamu vizuri kwamba hekima ya Mungu ni tofauti kabisa na mawazo ya wanadamu. Angalia majibu ya Yesu Kristo dhidi ya watu walio mwendea kwa nia ovu (**Luka 20:24-26**) hawa watu wanashangaa majibu ya Yesu kwani hayatokani na akili za kibinadamu, **angalia mawazo ya Yusufu wakati anafikiria kumwacha Mariam kumbe mawazo ya Mungu yalikuwa tofauti kabisa** (hapa utaona hekima ya Neno la maarifa na Hekima kwa pamoja, **Mt 1:18-21**) tena angalia hekima ya Mfalme Sulemani kwenye kesi ya wanawake wawili waliokuwa wanagombania mtoto (**1Wafalme 3:16-28**), angalia mfano wa mtume Petro Mungu alipompa majibu kwa Kornelio (**Mdo 10**). Katika habari ya Anania kwa Sauli tunaona Mungu anamfunulia Anania neno hekima kuhusu Sauli (**Mdo 9:15-16).** Angalia unabii wa Agabo **(Mdo 11:27-30),** Angalia uwezo wa Yusufu kutafsiri ndoto **(Mwz 41:25-39).**
   - **Kupambanua Roho:** Siyo hali ya kuhisia au kuhukumu wengine kwa hisia bali ni kujua mpango kamili wa Mungu juu ya mtu au wewe binafsi n.k. Jaribu kufikiria, zipo ndoto za Mungu na shetani naye anatoa ndoto kwa watu na zipo ndoto za

kawaida katika maisha ya kila siku. Je, utatambuaje ndoto iliyobeba mpango wa Mungu? bila shaka upambanuzi wa Roho unahitajika. Karama ya kupambanua Roho inampa mtu kufahamu kwa uhakika mapenzi ya Mungu katika ulimwengu wa Roho. Angalia utambuzi wa Anania kuhusu kumwendea Sauli, Anania alitambua kuwa yule alikuwa ni Yesu, utambuzi wa Petro juu ya kumwendea Kornelio (**Mdo 10**). Jaribu kufikiria wakati ambapo Mungu anakupa maono fulani labda kufanya jambo la kanisa au mtu binafsi n.k kisha unapata uhakika bila shaka yoyote kwamba ni Mungu ndiye aliyesema na wewe na hivyo unafanya hilo jambo mpaka linakamilika kisha unapata amani moyoni mwako.

4. **KARAMA ZA NGUVU/UTENDAJI**

- Karama za kuponya
- Karama za matendo ya miujiza
- **Imani ya uvuvio**: Siyo imani ya kawaida ya kuamini Kristo na uweza wake. Imani hii Mungu humvuvia mtu katika mazingira ambayo siyo rahisi kuamini katika hali ya kawaida. Mfano: Imetokea mtu amekufa ghafla lakini Mungu amvuvia mtu imani kwamba huyo mtu hajafa na anafanya maombi mfu anafufuka. Hiyo imani siyo kawaida na haimanishi kwamba kila siku unaweza kuamini hivyo na ikatokea.